



## SHIRIKA LA MAGEREZA (SHIMA) TAARIFA KWA UMMA



### MRADI WA MACHIMBO YA CHOKAA WAZOHILL NA KOKOTO MSALATO

Shirika la Magereza (SHIMA) ni Shirika la Umma lililoanzishwa Mwaka 1983 kwa kifungu namba 3(1) cha Sheria ya Mashirika ya Umma Namba 119 ya Mwaka 1974 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2002. Shirika linaendesha miradi ya Kilimo na Mifugo, Viwanda vidogo vidogo, Shughuli za ujenzi na Uchimbaji wa Madini.

Shirika linapenda kuutangazia Umma fursa ya uwekezaji wa pamoja kupitia Mradi wa kuchimba Kifusi na Chokaa uliopo Wazo Hill, Boko jijini Dar es Salaam na pia mradi wa kuchakata kokoto uliopo Msalato Jijini Dodoma.

Fursa hii ni ya kuwekeza mtaji na kuendesha shughuli za kuchimba madini ya kifusi na chokaa eneo la Wazo Hill na pia shughuli za kuchakata mawe na kutoa mazao ya aina mbalimbali za kokoto kwa eneo la Msalato. Miradi hii ina leseni za uchimbaji wa madini husika.

Mradi wa kifusi na chokaa upo eneo la Gereza Wazo Hill, Boko – Dar es Salaam na Mradi wa Kokoto upo Kata ya Veyula, Msalato -- Dodoma.

Taasisi na Kampuni zenye nia ya kuwekeza zinakaribishwa kuwekeza pamoja na Shirika la Magereza kwenye miradi hii muhimu kwa uchumi wa Taifa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu taratibu za uwekezaji wa ubia wasiliana na Shirika la Magereza kwa kutumia barua pepe [corpsole@prisons.go.tz](mailto:corpsole@prisons.go.tz) na [ceo corpsole@prisons.go.tz](mailto:ceo corpsole@prisons.go.tz) na pia tembelea tovuti ya Shirika kwa anuani ifuatayo [www.shima.go.tz](http://www.shima.go.tz) au *Scan barcode* iliyo chini ya tangazo hili.

